Government of **Western Australia**
Department of **Health**
Public and Aboriginal Health Division

Swahili

HealthyWA
healthywa.wa.gov.au

Habari ya Chanjo

Soma habari chini hapa kwa uangalifu kabla kuweka saini kwa fomu ya ruhusa. Kujifunza zaidi angalia healthywa.wa.gov.au/immunisation

	Virusi vya Papilloma vya Binadamu (HPV)	Mkamba-pepopunda-kifaduro (dTpa)
Ugonjwa huu ni nini?	**Human papillomavirus (HPV)** ni virusi vya kawaida vinavyoathiri wote wanaume na wanawake. HPV ni ya kuambukiza sana na hadi 90% ya watu wanaojamiana wataambukizwa na HPV wakati moja katika maisha yao. Mwili huondoa ambukizo kwa kawaida na kwa aina nyingi ya HPV, hakuna dalili zozote. Hata hivyo, aina nyingine za HPV zinaweza kusababisha dutu ya sehemu ya siri na aina nyingine za virusi zinaweza kuendelea kuwemo mwilini na kwa miaka mingi, kusababisha saratani (kansa) ya mlango wa kizazi, sehemu ya siri (uuke, vulva, uume) mkundu, mwili na koo.	**Mkamba** ni ambukizo la bakteria lenye kuambukiza sana na kuwezekana kuondoa uhai linalosababisha matatizo makubwa ya kuhema, kuharibu kabisa moyo na kuharibu neva. **Pepopunda** ni ugonjwa mkubwa, mara nyingi wa jaala unaoathiri mfumo wa neva. Watu wanao pepopunda wanathirika na mishtuko yenye maumivu ya misuli, mitukutiko na kufunga tayo. Mishtuko hiyo ya ghafula inaweza kuathiri mwili mzima, kusabibisha kukosa hewa na kuharibu moyo. Hata na uangalizi makini wa kisasa, alimradi wengi kama mmoja wa watu 50 wanopata pepopunda watafariki. **Kifaduro**, au whooping cough, ni ugonjwa wa pumzi unaoambukiza sana na unaweza kuondoa uhai wa watoto wachanga. Karibu mmoja wa watoto wadogo 125 wenye umri chini wa miezi sita wanaopata kifaduro watafariki kutoka numonia au kuharibika ubongo. Vijana na watu wazima wanao kifaduro watapata dalili kama-mafua na wanaweza kukohoa sana kwa hadi miezi mitatu.
Ugonjwa huu unaeneza njia gani?	**HPV** inaeneza kwa njia ya kugusana ngozi-kwa-ngozi sehemu za siri wakati wa shughuli ya kingono na mtu ambaye ana virusi. Virusi vya HPV ni vidogo sana kwa hiyo vinaweza kupita mipusuko midogo sana ngozini. Havienezi kwa njia ya damu. Kondom zinatoa kinga kidogo kukinga HPV, kwa sababu hazifuniki ngozi zote za sehemu za siri.	Bakteria za **Mkamba** zinaweza kuishi mdomoni, puani, kooni au ngozini kwa watu wanaoathirika. Watu wanaweza kupata mkamba kwa njia ya kuhema bakteria ndani baada ya mtu aliyeambukizwa amekohoa au kupiga chafu. Watu wanapata mkamba pia kwa kugusana karibu na kutoka usaha mdomoni, puani, kooni au ngozini ya mtu aliyeambukizwa. **Pepopunda** inasababishwa na bakteria kutoka udongoni na mbolea. Bakteria zinaweza kuingizia mwili kupitia jeraha alimradi kidogo kama mchomo wa pini. Haiwezi kueneza kutoka mtu kwenda mtu. **Kifaduro**, au whooping cough, kinaeneza kwa rahisi wakati mtu aliyeambukizwa anapokohoa au kupiga chafu bakteria hewani zinazoweza kuvutwa hewa na wengine wa karibu. Kama hapati tibu, mtu anacho kifaduro anaweza kuambukiza wengine kwa hadi ya wiki tatu baada ya dalili zimeanza.

	Human Papillomavirus (HPV)	Mkamba-pepopunda-kifaduro (dTpa)
Je, chanjo ni usalama na kufaa?	Ndio, vipimo zaidi ya milioni 270 vya chanjo za HPV vimepewa duniani katika miaka kumi iliyopita, inasifiwa na Shirika la Afya Duniani, na ni salama na kuvumiliwa vizuri. Chanjo ya **HPV** inafanya kazi nzuri sana inapopewa wakati wa umri mdogo kwa sababu jibu la kinga lina nguvu sana na inafaa sana inapotumiwa kabla shughuli za kingono zimeanza. Chanjo ya HPV inafaa 85–100% kukinga aina kuu ya kuambukizwa na HPV ambayo kunasababisha kansa na dutu ya siri. Wanawake wote waliopokea chanjo ya HPV watahitaji bado kupimwa kila mara kwa kansa ya mlango wa kizazi kwa sababu chanjo hazikingi kila aina za HPV. Vipimo milioni vya chanjo hii vimepewa duniani; ni salama na kuvumiliwa vizuri. . Hii ni kozi ya vipimo 2 vya chango. Ni muhimu kijana yako apokee vipimo vyote viwili kuhakikisha anakingwa kabisa.	Chanjo ya dTpa inafaa sana kukinga mkamba na pepopunda na inafaa karibu 80% kukinga kifaduro. Chanjo hii ya ziada ina mikusanyo midogo zaidi haswa sehemu za mkamba na kifaduro kulingana na chanjo iliyopewa wakati wa utoto mdogo. Chanjo ya ziada ni salama na kuvumiliwa vizuri.
Nini ni athari inayowezekana na tufanye nini kama ikitokeza?	**Athari za kawaida** Maumivu/unyekundu/mwasho/kidondo kidogo mkononi papo mahali palipotumiwa sindano. Kupunguza athari, weka kitambaa chenye maji cha baridi kwenye eneo la kuathirika. **Athari zilizo kawaidia** Homa isiyo kali, kuhisi kuumwa, chefuchefu, kuumwa kichwani. Kupunguza athari, waathirika wanaweza kumeza Paracetamol kufuata maagizo kwenye lebo na kunywa majimaji ziada. Ikiwa homa ikiendelea, mwona GP yako. **Athari za adimu sana** Athari kubwa zinawezekana, lakini ni adimu. Mifano ni pamoja na kuvimba usoni au tatizo la kuhema. Kama dawa zozote, kuna uwezekano mdogo sana kwa chanjo kusababisha jeraha kubwa au kifo. Ikiwa athari ni kubwa au ikiendelea, tafuta msaada wa uganga mara moja, na wasiliana na hospitali ya eneo lako.	**Athari za kawaida** Halijoto kidogo (chini 38°C) Kupunguza athari, meza Paracetamol kufuata maagizo kwenye lebo na kunywa majimaji ziada. Ikiwa homa ikiendelea, mwona GP yako. Maumivu/unyekundu/mwasho/kidondo kidogo mkononi papo mahali palipotumiwa sindano. Kupunguza athari, weka kitambaa chenye maji cha baridi kwenye eneo la kuathirika. **Athari za adimu sana** Brachial neuritis (uvimbe wa neva mkononi, unaosababisha udhaifu au uganzi). Athari kubwa zinawezekana, lakini ni adimu. Mifano ni pamoja na kuvimba usoni au tatizo la kuhema. Kama dawa zozote, kuna uwezekana mdogo sana kwa chanjo kusababisha jeraha kubwa au kifo. Ikiwa athari ni kubwa au ikiendelea, tafuta msaada wa uganga mara moja, na wasiliana na hospitali ya eneo lako.

Kutungwa na Kurugenzi ya Kudhibiti Magonjwa wa Kuambukiza
© Idara ya Afya 2019

Haki ya kunakili ya habari hii ni ya Jimbo la Western Australia isipokuwa imeelezwa tofauti. Badala ya kutumia kwa sababu ya kusoma kibinafsi, utafiti, zungumzo au ukaguzi, kama inavyoruhusiwa na utajiwa *Sheria ya Haki ya Kunakili 1968*, hakuna sehemu inayoruhusiwa kupigwa nakala au kutumiwa tena kwa sababu yoyote bila ruhusa ya mwandishi ya Jimbo la Western Australia

IMM-013216 JUN'19